

DAVID KAFULIHA (MB),

S.L.P 20,

14/07/2014,

UVINZA

DK, EDWARD HOSEA,

MKURUGENZI WA TAKUKURUA,

DAR ES SALAAM,

TANZANIA

Ndugu,

YAH: MAELEZO YANGU YAKIAMBATANISHWA NA VIELELEZO KUHUSU TUHUMA ZA UFISADI WA FEDHA ZA UMMA NDANI YA AKAUNTI YA TEGETA ESCROW CHINI YA BANK KUU YA TANZANIA.

UTANGULIZI

Utakumbuka kwamba kikao cha bunge la bajeti kwa mwaka wa fedha 2014/15, Nikichangia hotuba ya Waziri Mkuu nilijenga hoja kutaka uchunguzi wa Bunge kupitia Kamati teule ufanyike kuhusu tuhuma za ufisadi zinazohusisha kiasi cha dola 270millioni (zaidi ya 400billion) zilizopaswa kuwa ndani ya Akaunti hiyo sanjari na kiasi cha dola 122millioni (200billion) zilizokwishaolewa na kupewa kampuni ya PAP inayomilikiwa na Singasinga ajulikanye kwa jina la Harbinder Singh Sethi.


Katika maelezo yangu nilibainisha wazi kuwa viongozi wa juu serikalini kama Waziri wa Nishati na Madini, Waziri wa Fedha, Gavana wa Bank Kuu, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Katibu Mkuu Nishati na Madini, na Mkurugenzi wa Shirika la Ugavi wa Umma Tanzania wanapaswa kuchunguzwa. Hii ni kwa kuzingatia ushiriki wao wa moja kwa moja na wakati mwingine ushiriki wa Ofisi zao kama inavyojitokeza kwa waziri wa Fedha.

Kwa kuzingatia mjadala mkali ulioibuka nchini kuhusu tuhuma hizi za ufisadi huu, Kwa nyakati tofauti, Waziri Mkuu na Spika wa Bunge waliomba Bunge likubali PCCB na CAG kufanyia uchunguzi tuhuma hizi badala ya Kamati teule ya Bunge kuchunguza.

Aidha, Spika wa Bunge Anna Makinda kupitia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anielekeza nifikishe taarifa hizi kwa PCCB na CAG.

KWANINI NILISHAURI BUNGE LICHUNGUZE BADALA YA CAG NA PCCB

Nilipendekeza Bunge lichunge badala ya CAG na PCCB kwasababu zifuatazo;



1. PCCB ni chombo chenye jukumu zito lakini kisicho na meno kuweza kukabili rushwa inayohusu vigogo wakubwa serikalini kwani mwamuzi wa mwisho kuhusu uchunguzi ni Ofisi ya DPP ambaye amekuwa akitupilia mbali kesi nyingi tu kutokana na mamlaka aliyonayo kikatiba.

2. Malalamiko ya Ofisi ya PCCB kuhusu Ofisi ya DCI kukwamisha ufanisi wa vita dhidi ya rushwa ni ushahidi tosha,

3. Taarifa zilizopata kuvuja kwenye mtandao wa wikleaks kuwa Mhe Rais anakwamisha mambo mengi kuhusu vita ya ufisadi pia ni ushahidi mwingine

4. Uzoefu kwamba taarifa nzuri zinazofanyiwa uchunguzi kuhusu msingi wa ufisadi huu wa ESCROW ambayo ni IPTL kukaliwa na Ikulu bila kufanyiwa kazi. Unakumbuka Dr Hosea kuwa taasisi yako katika miaka ya 2000 ukiwa Mkurugenzi wa Uchunguzi kabla hujawa Mkurugenzi Mkuu ulipata kuchunguza kuhusu ufisadi wa mkataba wenyewe wa IPTL namna ulivyofikiwa kifisadi lakini pamoja na kufanya kazi hiyo nzuri Ikulu haikuchukua hatua dhidi ya wahusika na haitegemei kuchukua hatua i, Wewe unafahamu kuwa ripoti hiyo ingetosha kuwa ushahidi katika Mahakama ya ISCID kuweza kubatilisha mkataba wenyewe wa IPTL unaonyonya uchumi wan chi hii kwa muda mrefu, lakini Ikulu ilikalia kimya ripoti hiyo yenye vigogo waliohusika tangu mwanzo mpaka leo.


Kwakuwa nilijua Ikulu inao uzoefu wa kukalia kimya ufisadi huu wa IPTL tangu miaka hiyo, Na kwakuwa nilijua namna ufisadi huu ulivyofanyika mbele ya macho ya Kiongozi Mkubwa kama Katibu Mkuu Kiongozi, nilipoteza imani kama kweli PCCB inaweza kulichunguza jambo hili na matokeo ya uchunguzi yakazaa matunda. Niliamini itafunikwa kabatini Ikulu kama ambavyo ripoti kadhaa zinazohusu uchafu wa vigogo wan chi hii zinavyofungiwa Ikulu au kwa PCCB yenye kushindwa kutimiza wajibu wake kama ilivyojitokeza kwenye ufisadi wa RICHMOND..

6. Aidha pia uzoefu unaonesha kuwa pamoja na taarifa makini za CAG lakini ilipokuwa suala la kuchunguza ufisadi uliofanywa na aliyekuwa Katibu Mkuu wizra ya Nishati na Madini Bwa Jairo ambaye awali ufisadi wake ulibarikiwa na Ofisi ya Katibu Mkuu Kiongozi Ikulu wakati Mhe Luhanjo, CAG alikuja na ripoti mbovu ambayo ilimsafisha Jairo kama alivofanya Katibu Mkuu kiongozi awali. Ndio maana nilipata mashaka kama kweli CAG atakuwa huru kiasi cha kuchunguza jambo hili hasa ikizngatiwa kuwa linamuhusisha Katibu Mkuu Kiongozi Kwa maana alikuwa na taarifa za uchafu wote uliofanywa kila hatua kwani barua zote zilizohusu ufisadi huu kutoka wizara ya Nishati nakala ilipelekwa kwa Katibu Mkuu Kiongozi Mhe Omben Sefue

MAENEO YANAYOASHIRIA UFISADI

1. HUKUMU YA JAJI UTAMWA HAIKUHUJU FEDHA NDANI YA ESCROW

Kwa mujibu wa maelezo ya Waziri wa Nishati na Madini Bungeni pamoja na barua ya wizara ya Nishati na Madini iliyosainiwa na Katibu Mkuu Bw Eliakim Maswi kwenda kwa Gavana wa Bank Kuu na naka la kwenda kwa; Mwanasheria Mkuu wa serikali, Katibu Mkuu Hazina pamoja na Katibu Mkuu Kiongozi ikulu kuhusu kutoa fedha hizo, ilibainishwa kuwa msingi ulikuwa hukumu ya Mahakama Kuu ya



Septemba 5, 2013 chini ya Jaji Utamwa. (rejea barua hiyo yenye Ref.No.SAB.88/417/01/5 iliyorejea makubaliano ya IPTL na Wizara ya Nishati na Madini ambapo katika makubaliano hayo ya tarehe ya Oktoba 21, 2013 Wizara ya Nishati na Madini ilikubali kutoa fedha yote ndani ya ESCROW akaunti na kuipa kampuni ya IPTL/PAP)

Hata hivyo, kwa mujibu wa hukumu hiyo, Pamoja na ukweli kuwa ilisema kampuni ya PAP ipewe mali zote za IPTL haikusema kama fedha za ESCROW ni sehemu ya mali za IPTL. Pia Hukumu hiyo haikutaja kabisa kuhusu fedha hizo kwa namna yoyote. Pia fedha za ESCROW haikuwa sehemu ya maombi ya mfungua kesi.

Kwa msingi huo, Muhtasari wa kikao kati ya PAP na TANESCO ambacho kilifanyika Oktoba 8, 2013 Kunduchi Beach Hotel & Restaurant kuhusu fedha hizo ulikuwa batili na kikao chenyewe kilikuwa batili kwakuwa katika sehemu ya utangulizi kilitumia hukumu hiyo ya Septemba 5, 2013 kuhafalisha kutoa fedha na kuipa kampuni ya IPTL/PAP wakati hukumu ile haikuhusu kabisa fedha hizo.

Aidha, Kama wizara ingejitetea kwamba ilitafsiri hukumu ya Jaji Utamwa, bado ingekuwa na kosa kwani sio kazi ya wizara wala Mwanasheria Mkuu wa Serikali kutafsiri hukumu. Kazi ya kutafsiri hukumu ni kazi ya mahakama yenyewe kisheria.

2. UHAMISHAJI WA HISA ASILIMIA 70 ULIKUWA WA KUGHUSHI NDIO MAANA UNACHA MASWALI

Nyaraka nilizoambatanisha za TRA, zinaonesha kwamba Kampuni ya Mechmar iliuzia hisa zake ambazo ni asilimia 70 ya IPTL kwa kiasi cha Tsh6million kwa kampuni ya PIPERLINK tarehe ya Oktoba 15/11 2013 na badae tarehe ya Oktoba 30, 2013 kampuni ya PIPERLINK ikauza hisa hizo kwa kampuni ya PAP inayomilikiwa na Singasinga huyo Bw Singh Sethi kwa dola 300,000/ (Tsh 480million) zinazonesha kuwa kwa pamoja kampuni hizo mbili zilizouza hisa zililipa capital gain tax tarehe inayofanana, yaani Disemba 6, 2013. Hili lina mapungufu ya aina NNE;

Kwanza ni swali la kawaida inawezekanaje asilimia 70 ya hisa za kampuni ya IPTL inayomiliki mtambo wa 100MW, jengo pamoja na mkataba ziuzwe kwa million 6 awali kutoka Mechmar kwenda PIPERLINK na badae 480million kutoka PIPERLINK kwenda PAP?

Pili, asilimia 30 ya hisa za IPTL ziliuzwa kwa dola 75million (sawa na 120billion), iliwezekanaje hisa za kampuni hiyo hiyo ziuzwe kwa bei ndogo chini ya nusu billion?

Tatu, tarehe ambazo zinaonesha hisa hizo kuhamishwa kutoka MERCHMAR kwenda PIPERLINK na badae kutoka PIPERLINK kwenda PAP ni kipindi ambacho asimilia 100 za kampuni yote ya IPTL zilikuwa chini ya Liquidation Receivership, na hivyo kisheria isingewezekana kuuza hisa

Nne, PAP anayedai kuwa ni mmiliki halali wa asilimia 70 ya hisa hakuonesha share certificate ambao ni uthibitisho wa msingi wa umiliki wa hisa

Tano, Ni uwezekano wa Kampuni hizo mbili tofauti yaani Mechmar na PIPERLINK zifanye biashara ya kuuza hisa kila mmoja auze ndani ya mwezi mmoja yaani Oktoba 15/11 2013 na zote zilipe kodi siku moja yaani Disemba 06, 2013 wakati hisa ni zilezile za IPTL ambazo kampuni hizo zilimiliki kwa nyakatii tofauti?

Sita, Kwa mujibu wa sheria ya Fedha, Finance Act 2012, umiliki wa hisa unakamilika baada ya kulipwa kwa capita gain tax. Kwakuwa capital gain tax kwa mauzo ya asilimia 70 za hisa yalifanyika Disemba 6, 2013 maana yake kampuni ya PAP ilikuwa mmiliki halali wa IPTL baada ya muda huo, ni kwa msingi huo, hata kama matumizi ya hukumu ya Jaji Utamwa yangekuwa sahihi, bado uamuzi wa kumpa fedha za escrow Novemba 28 2013 wakati hisa ununuzi umekamilika Disemba ni kielelezo tosha kuwa kampuni ya PAP ilipewa kimakosa sio tu fedha za ESCROW bali pia mali zote za IPTL kwa maana ya mitambo na majengo kabla ya kuwa mmiliki halali. Kwanini Awe mmiliki halali Disemba 6 lakini apewe mali za IPTL na fedha za escrow tangu Novemba 2013? *kaela*

UMILIKI WA HISA ASILIMIA 30 ULIKUWA NA UTATA


Kampuni ya PAP ilisaini makubaliano na kampuni ya VIP ambayo inamiliki asilimia 30 za IPTL. Makubaliano yao ilikuwa VIP impe share certificate ya asilimia 30 PAP kisha PAP imlipe asilimia 10 ya mauzo kisha ndani ya wiki mbili amalize malipo lakini ukweli kilichotokea ni kuwa malipo ya zaidi ya dola 67 milioni ambayo ni asilimia 90% ya bei yote ya mauzo ya asilimia 30% za IPTL zilikuwa zinamilikiwa na VIP zililipwa baada ya Disemba 6, 2013 ikiwa ni tayari kampuni ya PAP ilikuwa imeshapokea fedha za ESCROW. Hii maana yake PAP ilichukuwa fedha za ESCROW 200 billioni na kasha kuzitumia hizo kufanya manunuzi ya share.

Aidha, haiingii akilini kwa mwekezaji makini afanye maamuzi ya kununua asilimia 30% za kampuni ya IPTL yenye mitambo ya kizamani na yenye miaka takribani 20 tena kampuni yenye rekodi ndefu ya Ufisadi na madeni lukuki ndani na nje ya nchi kwa dola 75 milioni wakati mitambo mipya yenye ubora zaidi ya hiyo bei yake ni takribani dola 100 milioni. Uamuzi huu unashiria kwamba mmiliki wa PAP hakuwa na lengo la kuwekeza bali kupora fedha za ESCROW kwa kushirikiana na vigogo serikalini.

BIASHARA HII ILIONEKANA YA WALAKINI NDIO MAANA BOT IKALAZIMISHA PAP INDEMNITY TAREHE OKTOBA 27, 2013

Katika mazingira yanayoashiria ama Gavana alishinikizwa kutoa fedha ya ESCROW au alishiriki uchafu kwa dhamira ni uamuzi wa Gavana kuelekeza PAP isaini mkataba wa kubeba dhamana kwa lolote litakalotokea kuhusiana na uamuzi wa kutoa fedha hizo. Huu ni ushahidi wazi kuwa Gavana aligundua kuna walakini badala ya kuhakikisha anaokoa nchi dhidi ya hasara ya ufisadi huu yeye akamua aelekeze INDEMNITY isainiwe kama njia ya kujitoa lawama. Huku ni kutowajibika na sio mfano wa uendeshaji wa taasisi kubwa zinazohitaji viwango vya juu vya uadilifu kama BOT


Aidha Gavana na Katibu Mkuu wa wizara ya Nishati na Madini wamepokea INDEMNITY iliosainiwa na PAP na IPTL Oktoba 27, 2013 kwa lengo la kuchukua fedha za akaunti ya ESCROW, tahehe hiyo ilikuwa kabla mchakato wa uhamishaji wa hisa kutoka IPTL kwenda PAP haujakamilika hivyo kisheria kisheria ulikamilika Disemba 6, 2013 baada ya kulipwa kwa kodi (capital gain tax)



MFULULIZO WA UONGO WA SERIKALI NI KIELELEZO CHA WALAKINI WA BIASHARA HII

Ndani ya kipindi cha Bunge la Bajeti, kwa nyakati tofauti, Waziri wa Nishati na Madini na Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Waziri Mkuu walitoa taarifa za kupotosha hali inayoweza kutafsiriwa kuwa hakukuwa na nia njema katika uamuzi wa kutoa fedha hizi.

1. Mara ya Kwanza Waziri Mkuu wakati akifanya majumuisho ya bajeti ya Ofisi yake kwenye bunge la bajeti lililomalizika alisema fedha za ESCROW sio za serikali labda pengine serikali ipate kodi tu. Huu ulikuwa upotoshaji wa kiwango cha juu kwa mamlaka ya juu kama Waziri mkuu kwani msingi uliophelekewa fedha hizo ziwekwe akaunti hiyo ya ESCROW haujapatikana na hivyo fedha hizo zimepewa PAP kabla ya kumalizika kwa mgogoro ambao mpaka sasa unaendelea kwenye Mahakama hiyo ya usuluhishi wa migogoro ya kibiashara ISCID. Unaweza kurejea barua ya Tanesco ya tarehe Mei7, 2014, yenye Ref 427/IPTL /5/2014 inayohusu ushiriki wa TANESCO kwa kesi hiyo ambapo iliomba kuongezewa muda wa kufanya hesabu upya kubaini bei sahihi ambayo TANESCO inastahili kuilipa IPTL.
2. Waziri wa Nishati na Madini alisema Fedha kwenye Akaunti ya ESCROW sio za Serikali bali ni za kampuni binafsi na kusisitiza kuwa uamuzi wa wizara yake na serikali kwa ujumla kuzitoa na kumkabidhi kampuni ya IPTL/PAP ulikuwa uamuzi wa mahakama. Kama nilivyoeleza hapo juu kwamba hukumu ya Jaji Utamwa ya Septemba 2013 hakuna mahala imesema fedha ESCROW ama ni mali ya IPTL wala hakuna mahala imelekeza PAP ipewe fedha hizo .
3. Waziri huyu huyu wa Nishati na Madini alibainisha kuwa sababu nyingine ya kutoa fedha hizo na kuwapa kampuni ya PAP ni ili kuondokana na kesi za muda muda mrefu ambazo zinaigharimu serikali kiasi kikubwa cha fedha. Huu ni uongo mwingine kwakuwa wakati Waziri anasema uamuzi ule unaiondoa serikali kwenye kesi za IPTL za muda mrefu, Mei12, 2014, Mkurugenzi wa TANESCO ameandika barua kwenda Mahakama ya ICSID akifahamisha kuendelea na kesi ya IPTL iliyoko mahakama hiyo ambapo pia ilihusu kuwatambulisha mawakili wa TANESCO katika mahakama hiyo(kampuni za uwakili zilizotambulishwa ni CRAX LAWS PARTNERS IN ASSOCIATION WITH R.K RWEYONGEZA &CO na kampuni ya ADVOCATES AND KELLERHALS ANWALTS ATTORNEY S AT LAWS) .Kwanini serikali inatengeneza visingizio vya uongo kuhalalisha uchotwaji huu wa fedha kinyume cha taratibu?
4. Mwanasheria Mkuu wa Serikali alisisitiza bungeni kuwa fedha hizo ni za kampuni binafsi na sio za serikali na kusisitiza kuwa msingi wa kufungua akaunti ya ESCROW ilikuwa ni kutokuelewana baina ya wabia wa kampuni ya IPTL yaani Mechmar (70%) na VIP mwenye 30%. Hapa Mwanasheria Mkuu wa Serikali alisema uongo kwani kwa mujibu wa Mkataba wa ESCROW uliosainiwa mwaka 2006 msingi wa kufungua akaunti hii ilikuwa mgogoro kuhusu malipo ambayo IPTL inatoza Tanesco kuwa ni makubwa kinyume cha mkataba, na ushahidi zaidi kuhusu ukweli huo ni hukumu ya awali ya ICSID ya Februari 2014 iliyoelekeza pande mbili zifanye hesabu upya kubaini kiasi halali ambacho TANESCO ilistahili kulipa kama Capacity Charge tangu mwanzo wa utekelezaji wa mkataba yaani mwaka 2002.



UKWELI NI NINI KUHUSU UAMUZI WA KUMPA PAP FEDHA ZA ESCROW

Tofauti na sababu zinazotolewa na Wizara ya Nishati na Madini ndani na nje ya bunge, ukweli ni kwamba fedha za ESCROW zilitolewa BOT kwa makubaliano baina ya wizara ya Nishati na Madini kwa upande mmoja na IPTI/PAP kwa upande wa pili(rejea muhtasari wa kikao chao cha tarehe). Na ni msingi huo uliophelekea Katibu Mkuu wizara ya Nishati na Madini kumwandikia barua gavana wa BOT Prof Benno Ndulu kumwelekeza atoe fedha hizo kwa IPTL akisisitiza kuwa ni maelekezo ya wizara yake yanayobarikiwa na Mwanasheria mkuu wa Serikali ambapo nakala ya barua hiyo ilikwenda pia kwa Katibu Mkuu Kiongozi Ikulu Bw Omben Sefue. Kwa maelezo ya muhtasari na barua hiyo Wizara ya Nishati na Mwanasheria Mkuu wa Serikali walielekeza fedha yote ya ESCROW kwa maana ya dola 270million zipewe kampuni ya IPTL/PAP.


SERIKALI ILIKUWA NA TAARIFA KUHUSU UTAPELI WA MMILIKI WA KAMPUNI YA PAP KWANINI HAIKUFANYA UCHUNGUZI KABLA

Kwa mujibu wa barua ya kampuni ya VIP ambayo ililipwa malipo yake yote ya kuuza asimilia 30 ya hisa zake kwa PAP baada ya PAP kuchukua fedha za ESCROW, barua hiyo inaonesha wazi kuwa Kampuni ya VIP ilikuwa imeshaeleza BOT na serikali nzima kwa ujumla kuhusu mashaka ya uadilifu wa kampuni hiyo ya PAP. Rejea barua yake iliyopokelewa BOT Disemba6, 2013 ikikumbusha barua ya Novemba 28, 2013 kuhusu hatari ya serikali kuingia kwenye matatizo endepo itampa fedha hiyo ya ESCROW kampuni ya PAP. Kwa hali ya kawaida, barua ile ilitosha kuifanya BOT na Serikali ione umuhimu wa kuchunguza kwa kina zaidi kuhusu mchakato mzima na uadilifu wa kampuni yenyewe yan PAP sanjari na mmiliki wake ambaye tayari kuna taarifa za mashaka kuhusu uadilifu wake kama mwekezaji katika nchi hizi za Afrika.

KWANINI WIZARA ILISHINDWA KUTEKELEZA HUKUMU YA MAHAKAMA YA ICSID YA FEBRUARI 2014 WAKATI ILIKUWA USHINDI KWA TAIFA?

Kwa mujibu wa hukumu ya awali iliyotolewa na Mahakama ya Kimataifa ya usuluhishi wa migogoro ya kibiashara, Mahakama ambayo ni sehemu ya Mkataba kati ya IPTL na TANESCO kwa mujibu wa kifungu cha 18.3(a)


Mahakama hiyo ilielekeza Serikali/TANESCO na IPTL/STANDARD CHARTERED BANK ndani ya siku90 kufanya upya hesabu za bei za umeme baada ya kubaini kuwa TANESCO ilikuwa ikitozwa zaidi kinyume cha mkataba. Maelekezo hayo ndiyo yangetumika kujua ni kiasi gani TANESCO imeibiwa kufuatia udanganyifu wa IPTL kwenye mtaji tangu mwaka 2002 ilipoanza kuuzia TANESCO umeme na kudai kuwa imewekeza dola 38millioni kama equity (asilimia 30 ya mtaji) wakati iliweka dola 50 tu. Kama kwa hesabu ya sasa capacity charge inalipwa dola 2.6millioni kwa mwezi, kwa mkataba wa miaka 20, hii tafsiri yake ni kwamba asilimia 30 za capacity charge ingepunguzwa ambapo kwa mwezi TANESCO ingeokoa sio chini ya dola 780000 kwa mwezi sawa na dola 187.2millioni(308.9billioni kwa muda wote wa mkataba).



MWISHO

Napenda kuwahakikishia ushirikiano madhubuti, na nipo tayari kwa swali lolote litakalohusiana na maelezo yangu na mengineyo kadiri mamlaka za uchunguzi zikavyohitaji kwa lengo la kufanikisha uchunguzi huu. Nilisoma hadidu za rejea ambazo Bunge na Ofisi ya waziri Mkuu zimetoa kuhusu uchunguzi huu, imelekezwa kwamba uchunguzi wa suala hili uanzie mwaka 2006 ilipofunguliwa ESCROW AKAUNT mpaka ilipofungwa. Nashauri uchunguzi ufanyike tangu TANESCO ilipoanza kununua umeme IPTL kwa maana ya mwaka 2002 kutokana na hoja kwamba TANESCO ilianza kupunjwa tangu mwaka 2002 ilipoanza kununua umeme na kulipa capacity charge kubwa kinyume cha mkataba kutokana na udanganyifu wa mtaji(equity).

Pamoja katika utumishi bora;



DAVID ZACHARIA KAFULILA (MB),

MBUNGE WA KIGOMA KUSINI,

NAKALA:

SPIKA WA BUNGE

MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI (CAG)